

**Dr. Wilfred D. Kiboro**
*Mwenyekiti*

# Taarifa Ya Mwenyekiti

**Wapendwa Wenyehisa,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ni furaha yangu kuwapa ripoti ya matokeo ya kifedha na yale yasiyo ya kifedha ya Kampuni ya mwaka uliokamilikia tarehe 31 Desemba, 2022.

### Mazingira ya Kiuchumi na Biashara

2022 ulikuwa ni mwaka mgumu kwa mtazamo wa kiuchumi na kibiashara. Vigezo vikuu vilivyosababisha kudorora kwa uchumi katika ukanda wa Afrika Mashiriki vilikuwa ni pamoja na ongezeko la gharama ya mishahara kwa wafanyakazi, kushuka kwa thamani ya sarafu na kuongezeka kwa deni la umma.

Uchumi wa nchi za Afrika Mashariki ulipungua pakubwa huku ukuaji wake nchini Kenya ukipungua zaidi kuliko ilivyokadiriwa awali kutoka 7.6% mwaka wa 2021 hadi 4.8% mwaka wa 2022; GDP ya Uganda ilikuwa 4.6% mwaka 2022 ikilinganishwa na 6.0% mwaka wa 2021 na GDP ya Rwanda ilipungua kutoka 10% mwaka 2021 hadi 6.9% mwaka 2022. Uchumi wa Tanzania ulikua kidogo kutoka 4.3% mwaka 2021 hadi 4.6% mwaka 2022. Hii ilisababishwa na kupanda kwa bei za bidhaa kutokana na ukame na vita, kupungua kwa mapato, na kupungua kwa matumizi katika sekta ya kibinafsi wakati wa uchaguzi.

Hali nchini Kenya, ambayo inachangia 70% ya mauzo ya Shirika ilikuwa mbaya zaidi kwa sababu ya ukame ambao ulikumba nchi hii baada ya miaka 40 na kuathiri zaidi ya watu milioni 5 na kusababisha athari mbaya kwa utoshelevu wa chakula na hali ya maisha. Hii ilisababisha kujikokota katika ukuaji wa sekta muhimu za uchumi ambazo ndizo wateja wetu wakubwa wa utangazaji. Sekta ya kilimo inayochangia 21.2% ya GDP ya Kenya ilipungua kutoka -0.4% mwaka 2021 hadi -1.6% mwaka 2022. Sekta ya elimu pia iliathirika vibaya huku zaidi ya shule 7,000 za kibinafsi zikifungwa katika miaka 4 iliyopita, hali hii ikiakisi matatizo yanayokumba sekta kuu kama hiyo wakati kuna matatizo ya kiuchumi yanayosababishwa na tandavu ya UVIKO-19.

**Millioni 5**

**Hali nchini Kenya, ambayo inachangia 70% ya mauzo ya Shirika ilikuwa mbaya zaidi kwa sababu ya ukame ambao ulikumba nchi hii baada ya miaka 40 na kuathiri zaidi ya watu milioni 5 na kusababisha athari mbaya kwa utoshelevu wa chakula na hali ya maisha.**

Hali iliyoelezwa hapo juu, Afrika Mashariki imeakisi changamoto zilizopo katika kurejea kwa uchumi wa dunia. Ukuaji halisi wa GDP ya dunia ulipungua hadi 3.4% mwaka 2022 kutoka ukuaji wa 6.0% mwaka 2021. Hii ilisababishwa na kukazwa kwa sera za kifedha baada ya UVIKO-19, kuibuka tena kwa UVIKO-19 nchini China na vita baina ya Urusi na Ukraine ambavyo vilisababisha bei za kawi na vyakula kupanda pakubwa.

Katika mazingira yaliyoelezwa hapo juu ya kufanya kazi, sekta ya habari ya ukanda huu ilishuhudia pengine mojawapo ya miaka yake migumu zaidi katika historia huku baadhi ya vyombo vya habari ama vikifungwa au vikijipata katika hatari ya kuanguka. Vyombo vya habari viliendelea kukumbana na changamoto kutokana na vurugu za kidijitali, kiasi kikubwa cha madeni ya serikali, hali tete ya kisiasa na mashambulizi dhidi ya uhuru wa wanahabari katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kando na haya, ongezeko la bei ya mafuta na uchapishaji wa habari iliongeza pakubwa msingi wetu wa gharama. Shirika lilishughulikia changamoto hizi kwa kuendesha mageuzi yetu ya kidijitali kwa kufanya mabadiliko makubwa katika muundo wetu wa biashara na kutekeleza hatua madhubuti ya udhibiti wa gharama.

Licha ya hayo, taswira ni chanya huku kurudi kwa mvua na mazingira ambayo ni ya amani kwa jumla zikiwezesha kurejea haraka kwa shughuli za kiuchumi. Isitoshe, ushirikiano wa moja kwa moja wa kibiashara kati ya nchi za Afrika Mashariki na Ukraine haujaathirika pakubwa, kwa sababu Urusi na Ukraine zinachangia asilimia ndogo ya jumla ya bidhaa za biashara. Vilevile, watalii kutoka Ukraine na Urusi hawachangii mgao mkubwa wa soko la utalii la Afrika Mashariki. Ni jambo la kutia moyo kwamba sekta ya utalii inarejea katika ukanda huu.

### Mandhari ya Kisiasa

Kenya ilifanya uchaguzi mkuu wa 2022 ambao ulikuwa wa amani pakubwa na vurugu chache. Hata hivyo, kulikuwa na hali tete na hofu ikijumuisha mapambano makali mahakamani katika Mahakama ya Upeo hali ambayo ilisababisha kupungua kwa matumizi ya pesa ndani ya nchi na shughuli ya kiuchumi huku sekta ya kibinafsi ikiamua kutumia mbinu ya kutazama na kusubiri.

NMG ilichukua nafasi yake katika lengo lake la kuwa mshirika wa kuaminika kwa demokrasia za Afrika, mtetezi wa mtu wa kawaida katika kutangamana na serikali iliyo mamlakani, sauti ya utawala wa kisheria na kuheshimu haki za binadamu. NMG iliripoti kwa upana kuhusu uchaguzi huo kwa kutoa habari sahihi, zisizoegemea upande wowote na za ukweli kwa umma. Pamoja na mpango wetu wa *Mimi Mkenya, t*ulifuata mwongozo wa sera yetu ya uhariri kuleta habari kuhusu wawaniaji wote kwa usawa, uyakinifu lakini kwa ujasiri na kuwawajibisha viongozi katika baadhi ya masuala muhimu kwa taifa na watu wa Kenya. Hivyo ilikuwa inatia moyo kuona kuibuka kwa masuala ya kijamii na kiuchumi kama mambo yanayotiliwa maanani katika kampeni za uchaguzi.

Hata hivyo, wanahabari waliendelea kushambuliwa, kutishiwa na kuonewa wakati wa uchaguzi. Tulishirikiana na kufanya kazi kwa karibu na mashirika katika sekta ya habari kama vile Muungano wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari (MOA), Baraza la Habari la Kenya (MCK), Baraza la Wahariri, Muungano wa Wanahabri wa Kenya (KUJ), mashirika ya kijamii miongoni mwa wengine kukashifu mashambulizi hayo na kutoa mwito wa kukomeshwa kwake.

# Taarifa ya Mwenyekiti (inaendelea)

Kutokana na hayo, maudhui ya uchaguzi kwenye mifumo yetu yote yalisababisha ukuaji kwa 13% katika uwepo wetu wa kidijitali, na ongezeko la 65% katika jumla ya trafiki kwenye wavuti. *Nation.Africa,* ambayo ilipangisha kituo cha uchaguzi cha Shirika hili na kutoa matokeo ya uchaguzi kwa wakati halisi, ilikua kwa 44% katika watumiaji wa kipekee na ongezeko la 62% katika idadi ya watu waliotazama ukurasa wetu katika kipindi hicho cha uchaguzi.

Katika kipindi hicho, kama wanachama wa MOA, tulishirikiana na MCK na baraza la wahariri wa Kenya, kupanga Misururu ya Mdahalo wa Urais 2022 ili kwa pamoja kuweka utamaduni wa kuwepo Midahalo ya Urais kama mojawapo ya nguzo kuu ya demokrasia na mchakato wa uchaguzi kwa manufaa ya watu wa Kenya. Wakati wa midahalo hii, umma ilisikiliza wawaniaji na kutathmini mambo ambayo wangeyapa kipaumbele baada ya kuchukua hatamu za uongozi. Kwa njia hiyo, midahalo hii ilichochea uchaguzi uliojikita kwa masuala muhimu, ilitoa fursa kwa wawaniaji kushiriki katika mdahalo, kuingiliana na kushirikiana na kuwezesha Wakenya kufanya maamuzi ya busara.

Ninafurahi kusema kwamba ripoti nyingi za misheni za waangalizi wa uchaguzi wa Kenya zilipongeza nafasi ambayo vyombo vya habari vilichukua katika uchaguzi. Ripoti ya Mwisho ya Ujumbe wa Uangalizi wa Uchaguzi kutoka EU nchini Kenya ilisema kwamba 'kwa kuweka pamoja viwango vyote sita vya uchaguzi, vituo vya kibinafsi vya TV, vilitoa nafasi sawa za kuangazia mambo ya miungano miwili mikubwa'. Ripoti hiyo iliendelea kusema kwamba 'vyombo vya habari vilitoa ripoti zinazojali jinsia za watu na kuangazia wawaniaji wanawake kwa kuwapa nafasi ya kutosha'.

Mandhari ya kisiasa katika maeneo mengine ya ukanda wa Afrika Mashariki yaliendelea kuwa thabiti isipokuwa vita vinavyoendelea Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Tunashukuru uamuzi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizotuma Vikosi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACRF) kupambana na waasi na kurejesha hali ya kawaida nchini humo.

**billioni 7.3**

**Shirika hili lilipata mauzo ya shilingi bilioni 7.3 na faida ya kabla ya kodi ya shilingi bilioni 0.5**

### Mageuzi ya Shirika

Katika taarifa yangu ya awali, nilisema kwamba muundo wa kibiashara wa Shirika ulikuwa unafanyiwa mabadiliko makubwa ili kuliwezesha kugeuka kuwa kampuni ya kisasa ya maudhui ya kidijitali. Hakika, mnamo 2022, safari ya mageuzi ya NMG ilishika kasi kupitia utekelezaji wa miradi kadhaa muhimu ili kuitikia vurugu za kidijitali zilizokumba sekta ya habari. Shirika hili lilishirikiana na FT Strategies (idara ya ushauri wa usajili wa shirika la Financial Times lililo London) wataalamu ambao walifanikiwa kuleta mageuzi katika muundo wa kibiashara wa FT wakati wa vurugu kama hizo. Mipango hii ilijumuisha kufafanua wazi North Star ya Shirika, Mradi Jumlishi wa Chumba cha Habari na kuundwa kwa mkakati mpya wa maudhui.

Mradi wa North Star ulizinduliwa kwa lengo ya kukuza kwa muda mapato yetu ya kidijitali kwa miaka 5 ijayo kwa kufanya mageuzi na kuwa mfumo wa maudhui unaoaminika zaidi, wa kuwezesha na wa uvumbuzi barani Afrika. Mageuzi haya yamejikita kwenye utamaduni wa shirika, kipindi cha matumizi ya mteja, uwezo wa data na teknolojia, uvumbuzi wa bidhaa na uhamasisho kuhusu chapa. Kuhusiana na hili, ninafurahi kuwajulisha kwamba kuenda mbele Shirika litakuwa linafanya kazi ili kufikia North Star ijayo:

*"Kugeuka kuwa Mfumo wa Maudhui ya Kiuvumbuzi na Unaoaminika Zaidi Barani Afrika tena unaohamasisha Mitagusano Milioni 500 kila Siku na Kuleta Dola za Marekani Milioni 55 katika Mapato ya Kidijitali kufikia Mwisho wa 2027."*

Tumejitolea kuipa kipaumbele hadhira yetu katika kila tunachofanya, na mojawapo ya misingi ya hatua hii ni Mradi wa Ujumlishaji wa Chumba cha Habari. Kuleta pamoja talanta ya uhariri kwenye chumba chetu cha habari kutaimarisha shughuli za maudhui yetu na kina cha utaalamu wetu kwa manufaa ya mifumo na chapa zote, hivyo kufanya Shirika hili kuwa biashara yenye ushindani mkubwa hata zaidi. Awamu ya kwanza ya shughuli hii imekamilishwa na inahusu kufanyia mageuzi chumba cha habari ili kiwe na shughuli zinazoongozwa na matakwa ya hadhira na kuunda kwa pamoja muundo mpya wa kiidara ambao unaboresha tija ya chumba cha habari na kudumisha mtazamo unaoupa kipaumbele kufanya mambo kidijitali na mbinu ya uhariri inayomlenga mteja.

Kama kiendelezo cha Mradi Jumlishi wa Chumba cha Habari, pia tumeanza kufafanua mkakati wa maudhui wa NMG kutokana na matokeo ya utafiti mpana ambao ulichunguza mahitaji ya mteja, mchakato wa kuunda maudhui na utendaji wa maudhui kwenye mifumo yetu. Sasa tuna chapa kuu inayoongoza uundaji, uwasilishaji na uchumishaji wa maudhui yanayolipiwa kwenye mifumo yetu ya kidijitali.

### Matokeo ya Kifedha

Shirika hili lilipata mauzo ya shilingi bilioni 7.3 na faida ya kabla ya kodi ya shilingi bilioni 0.5 (2021 ilikuwa bilioni 7.6 na bilioni 0.7) Mazingira magumu ya biashara yaliyotokana na changamoto za msururu wa usambazaji wa bidhaa kote duniani yalisababishwa na vita baina ya Urusi na Ukraine, kupanda kwa bei ya bidhaa msingi, kuongezeka kwa gharama za mafuta na ukame ulioshuhudiwa kote katika ukanda huu uliathiri vibaya utendaji wa Shirika hili.

Shirika lilisajili ukuaji katika mapato ya kidijitali na linaendelea kutilia maanani uvumbuzi wa bidhaa kwenye vituo na mifumo yetu yote ili kufanya hadhira kununua, kushiriki na kuboresha uchumishaji wa bidhaa zetu nyingi za kidijitali. Hii itafanywa sambamba na kudumisha uwepo thabiti wa Shirika katika vyombo vya habari vya machapisho na matangazo kwa kuendelea kutoa maudhui ya aina yake na muhimu kwa hadhira zetu.

# **Taarifa ya Mwenyekiti** (inaendelea)

> **Katika muda wote wa uwepo wetu, Nation imesimama kidete na thabiti katika dhoruba kali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kufanya lengo letu muhimu la 'kuchochea jamii kwa njia chanya'.**

## Migao

Wakurugenzi wanapendekeza malipo ya mgao wa mwisho wa mapato ya hisa ya Shs 1.50 kwa kila hisa kwa mtaji wa hisa uliotolewa na uliolipiwa kikamilifu ambao umerekebishwa kwa ajili ya hisa za kifedha (hisa za 190,295,163 za kawaida kwa thamani ya Shs 2.5 kwa kila hisa), hii ikisubiri kuidhinishwa na wenyehisa wakati wa Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka. Hakuna mgao wa mapato ya hisa ya muda uliolipwa katika mwaka huu.

## Mpango wa Ununuzi wa Hisa

Bodi ya Wakurugenzi wa NMG waliamua kupendekezea washikadau wake kununua hadi asilimia kumi (10%) ya mtaji wa hisa yake uliotolewa na uliolipiwa kikamilifu (ambao umerekebishwa kwa ajili ya hisa za kifedha), katika Mpango wa Ununuzi wa Hisa Zake kwa mujibu wa vifungu vya sheria za Makampuni na Kanuni za Masoko ya Mtaji (Dhamana) (Ofa za Umma, Uorodheshaji na Ubainishaji), 2002. Hii itawapa washikadau wa NMG chaguo la kuuza uwekezaji wao na kupata pesa. Mpango wa Ununuzi wa Hisa unafuata kanuni na uidhinishaji wa mshikadau.

Ununuzi wa hisa hutokea wakati kampuni inanunua kutoka kwa wawekezaji wake sehemu ya hisa zake zilizotolewa. Ni mojawapo ya njia za kampuni kurudisha fedha kwa washikadau wake, kupunguza kwa ufanisi idadi ya hisa zilizotolewa na kuongeza haki za usawa za hisa yoyote moja. Ununuzi wa hisa hulenga kuwapa washikadau chaguo mbadala wa kuongeza thamani kutoka kwa uwekezaji wao.

## Uongozi katika Mawazo

Mwaka uliotangulia ulishuhudia Shirika kuimarisha nafasi yake ya uongozi katika kuendesha mazungumzo muhimu kupitia kuleta pamoja mijadala ya uongozi wa kimawazo yenye athari kubwa ili kuwezesha maendeleo ya ukanda huu na bara Afrika. Kuhusiana na hili, Shirika lilifanya misururu ya mijadala ya nchi mahususi. Nchini Kenya tuliandaa *Nation Leadership Forums (NLF)* kwa mwaka wa 6 kwa mpigo, *Kongamano la Kawi Endelevu* ambalo lilikuwa la kwanza kabisa na *SME Expo and Conference,* Onyesho la Kazi la *Nation-Huwaei.* Nchini Uganda, tuliandaa *The Economic Summit* huku nchini Tanzania tukiandaa Mijadala ya *Mwananchi Thought Leadership.* Mijadala hii ilishughulikia nyanja muhimu kama vile miji inayojali mazingira, ukosefu wa ajira kwa vijana, kilimo, elimu, afya, Biashara Ndogo na za Wastani (MSMEs), uchumi, utengenezaji bidhaa, teknolojia na nyinginezo.

Shirika liliendelea kutekeleza jukumu lake la kutoa taswira ya mustakabali wa bara la Afrika kama 'Media of Africa for Africa' kwa kuandaa makala ya nne ya *Tamasha la Kusi Ideas.* Mwaka jana, tamasha hilo lilirejea nchini Kenya katika jiji kuu chini ya mazingira mazito ya eneo la maarufu na lililolindwa la mazingira nchini Kenya, Msitu wa Karura. *Tamasha la Kusi Ideas,* ambalo kaulimbiu yake ilihusu, "Changamoto ya Mabadiliko ya Tabianchi: Kuchunguza Miitikio na Suluhu za Kiafrika" lilichunguza athari ya mabadiliko ya tabianchi kama tishio linalozidi kuwa kwa maisha na hali za maisha barani Afrika - kuanzia athari yake kwa utoshelevu wetu wa chakula hadi mipango na uvumbuzi wa Kiafrika unaohitajika ili kulinda bara hili. Makala haya yalifanyika tarehe 8 – 9 Desemba 2022, baada ya kongamano la COP-27, ambalo lilikuwa limeisha nchini Misri.

Kongamano hilo lilivutia wazungumzaji 50, kutoka kote barani Afrika. Liliungwa mkono kwa pamoja na William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya na lilihudhuriwa na Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Tanzania, Sultan Rahim Aga Khan, Aga Khan Development Network, Bi. Rosalinda Soipan Tuya, Waziri wa Mazingira na Misitu, Anne Waiguru, Mwenyekiti, Baraza la Magavana, Balozi Meg Whitman, Balozi wa Marekani nchini Kenya, Prof. Patrick Verkooijen, Afisa Mkuu Mtendaji Global Centre on Adaptation, miongoni mwa washikadau wengine ikiwa ni pamoja na wawakilishi kutoka jumuiya ya kidiplomasia, wataalamu, wavumbuzi, wanazuoni, wajasiriamali na wakuu wa sekta mbalimbali. Lilihudhuriwa na wajumbe 524 waliohudhuria ana kwa ana, wajumbe 3,449 waliohudhuria mtandaoni na Televisheni ikifikia watu milioni 1.83 na zaidi ya watumiaji millioni 28 kwenye mtandao wa kijamii.

## Ajenda ya Uendelevu

Katika muda wote wa uwepo wetu, Nation imesimama kidete na thabiti katika dhoruba kali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kufanya lengo letu muhimu la 'kuchochea jamii kwa njia chanya'. Miongo kadhaa baadaye, tunajivunia turathi hii ya kuunda thamani kwa jamii zilizo karibu nasi na bado tupo katika nafasi ya mbele ya kufanikisha hili na majukumu mengine ya kimaendeleo. Hakika, katika miongo sita iliyopita, NMG kupitia ushirikiano imewekeza rasilimali za kutosha kupitia mijadala ya uongozi, kampeni kali, muda hewani, nafasi kwenye magazeti, muda wa likizo kwa wafanyakazi, rasilimali za kifedha ili kutatua masuala ya kijamii kama vile mazingira, njaa, elimu, afya, na masuala mengine ya maendeleo ya jamii.

Hivyo, tunapoendelea na safari ya kuwa shirika linalojituma zaidi, linalolenga wateja na kuendeshwa na data, lengo la Shirika hili litaendelea kuwa nguzo katika kuendesha uendelevu wa biashara yetu kupitia kuleta manufaa ya kudumu katika jamii. Lengo ni kuendelea kudumisha Kampuni hii kama chaguo la kimkakati na la kudumu la mshirika.

Ni kwa sababu hii ambapo Wakfu wa Nation Media ulianzishwa kwa lengo la kuwezesha Shirika hili kuendesha mchango wetu na kuboresha mipango katika juhudi za kufikia



**Nchini Kenya tuliandaa *Nation Leadership Forums (NLF)* kwa mwaka wa 6 kwa mpigo, *Kongamano la Kawi Endelevu* ambalo lilikuwa la kwanza kabisa, SME Expo and Conference, Onyesho la Kazi la Nation-Huwaei.**

# **Taarifa ya Mwenyekiti** (inaendelea)

Malengo Endelevu ya Maendeleo katika nyanja za: Elimu na Kusoma na Kuandika; Usimamizi wa Mali Asili na Mabadiliko ya Tabianchi; Afya; Maendeleo ya Vyombo vya Habari; na Maendeleo ya Jamii kupitia Ujasiriamali na Misaada ya Kibinadamu. Wakfu huo ni msingi wa kitaasisi wa juhudi zetu za kuhakikisha uthabiti, mikakati ya kukusudia na yanayolengwa kupitia mbinu ya thamani ya pamoja ambayo itakuwa na ufikiaji mpana na kuleta mageuzi endelevu katika jamii.

Mojawapo ya masuala muhimu ambayo tunashikilia kwa dhati ni elimu, ambayo ni msingi wa Mpango wa Mradi wa Wakfu. Mpango wa Elimu na Kusoma na Kuandika ni mkakati uliozinduliwa kote nchini ambao ulibuniwa ili kujibu changamoto ya viwango vya chini vya masomo, viwango vya chini vya ufikiaji wa vitabu na kuendeleza utamaduni wa kusoma. Vilevile, kwa kuangazia ukweli kwamba sisi ni watumiaji wa habari za kuchapishwa, tunalenga kuendelea kutilia maanani mipango ya mabadiliko ya tabianchi kama vile kupanda miti ili kuendelea kupunguza viwango vya kaboni tunavyochangia. Tayari tumeshirikiana na mashirika kama vile Wakfu wa Green Blue Foundation Afrika, Family Bank, Huduma ya Misitu ya Kenya kwa ajili ya shughuli ya upanzi upya wa miti katika Milima ya Ngong na kaunti kama vile Machakos na Uasin Gishu kwa urejeshaji minara ya maji.

## Mabadiliko kwenye Bodi

Kulikuwa na mabadiliko fulani kwenye Bodi mwaka uliopita. Anwar Poonawalla alistaafu kwenye Bodi ya NMG. Poonawalla alijiunga na bodi hii kama mkurugenzi asiye mtendaji mnamo mwezi Juni 1989. Katika kipindi hicho alikuwa mwanachama wa Kamati ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu, Uteuzi na Utawala na Idara ya Wafanyakazi. Bodi inamshukuru kwa dhati Poonawalla kwa miaka 33 ya kujitolea kuhudumu kwa Bodi ambapo Bodi ilinufaika kutokana na uzoefu wake mpana katika utawala, usimamizi, fedha na uundaji wa mikakati.

## Watu Wetu

Mageuzi ya Shirika yanafanyika kwa kuweka mazingira mazuri ambapo timu yetu imewezeshwa kwa kupewa ujuzi unaofaa na teknolojia ya kuondoa ujuzi wa zamani, kujifunza ujuzi tena na kujifunza ujuzi mpya huku tukikuza NMG ya siku za baadaye. Kwa hivyo, tumeweka maanani

**Tunatambua kuwa mageuzi haya yanahitaji tufanye mabadiliko kutoka chapa hadi shirika linalowapa hadhira na wateja kipaumbele na kuhudumia wahafidhina na wanafanya mambo kidijitali kwa pamoja.**

katika kukuza utamaduni wa uwazi, wa huruma na jumuishi wenye matokeo bora zaidi ambao ni wa usawa, wa kirafiki na kuburudisha ambapo kila mtu katika shirika ni balozi wa ajenda ya mageuzi.

## Mustakabali Wetu

Katika ulimwengu ambapo hadhira imeegemea kufanya mambo ya kijamii kidijitali kwa dhati, njia ya pekee ya kuleta thamani kwao ni kufanya mageuzi ili kuwa shirika la habari la kiuvumbuzi linaloaminika ambalo linawafaa katika maisha yao kwa kuwa chombo kinacholeta maudhui ya kipekee, ya ubora wa juu kwa kuwarahisishia mambo kwa njia wanayopendelea. Tunatambua kuwa mageuzi haya yanahitaji tufanye mabadiliko kutoka chapa hadi shirika linalowapa hadhira na wateja kipaumbele na kuhudumia wahafidhina na wanafanya mambo kidijitali kwa pamoja.

Kuhusiana na hili, mustakabali wa Shirika ni kuendelea kufahamu mahali tunapohitaji kulitia maanani huku tukielewa mfumo ikilinganishwa na maudhui na vigezo visivyobadilika ikilinganishwa na vinavyobadilika. Hii inamaanisha kubadilisha njia zetu za kufanya kazi ili kukita data katika mbinu zetu za kufanya uamuzi na mbinu mpya za kuunda bidhaa zinazotuwezesha kukumbatia makosa (madogo) kwa kukosa haraka lakini kwa gharama tunayoweza kumudu. Hii pia itahusisha uvumbuzi upya wa hali yetu ya utumiaji ili kuunda maudhui ya kuwafaa watumiaji na kuendesha ushirikisho wa watu kupitia vifaa vya mkononi, kuongoza mwanamke(mwanaume) na mashine na kuwezesha watu na utamaduni wetu huku tukiongeza uwezo wetu wa uhandisi kupitia kuajiri talanta mpya.

Mustakabali huu utatupelekea kuchunguza njia za kuingia katika masoko mapya yanayoibuka. Ninafurahi kuripoti kwamba Shirika hili tayari limeanza juhudi hizi kwa kupanga kongamano la kwanza la *The EastAfrican Business Conference and Trade Fair* jijini Kinshasa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Kongamano hilo lilileta pamoja biashara na wakuu wa sekta mbalimbali kutoka kote katika ukanda wa Afrika Mashariki ili kuchunguza fursa za uwekezaji nchini DRC. Kuna fursa kubwa hata zaidi kwa biashara yetu nchini DRC kupanuka kutokana na hatua ya nchi hiyo kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Shirika hili tayari linaweka hatua za kuchunguza uwezekano huu na kuingia nchini DRC.

Bodi ina imani kubwa kwa usimamizi na wafanyakazi kufanikisha mustakabali huu mpya wa kimageuzi. Tumeona ahadi, ari na juhudi zinazoelekezwa katika kutoa taswira ya shirika mpya ambalo litaweka biashara katika nafasi thabiti na endelevu. Kampuni nyingine za habari kote duniani zimeweza kubadilisha na kuanza kufanya mambo kidijitali wakati kumekuwepo na vurugu na tuna matumaini kuwa NMG itafanikiwa katika juhudi hizi.

Ninataka kushukuru wafanyakazi wenzangu kwenye Bodi kwa ustahimilivu, kujitolea na maono yao. Bila shaka kujitolea kwao bila kutetereka na mchango wao umefanya Shirika kuendelea kuweka kasi katika safari yetu ya kufikia mageuzi.

Acha nimalize kwa kuchukua fursa hii kuwapa kongole usimamizi na wafanyakazi kwa juhudi, ari na kufanya kazi kama timu katika kufanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha si tu ahadi yetu bali pia kuweka Shirika katika nafasi nzuri kwa ajili ya kesho iliyo bora. Kwa washikadau wetu, washirika wa biashara, wateja wetu na washikadau wengine, sisi ni nyinyi na nyinyi ni sisi. Asanteni kwa kutuamini kufanikisha mambo yetu kila siku ya kuwepo kwetu.

Ahsanteni sana.

**Dkt. Wilfred D. Kiboro**


FOLLOW US
ON SPOTIFY!
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
Spotify
@Nation FM KE